

**OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI WA KAHAMA**

**Bugisha Sekondari
S.L.P 873
Kahama
Tarehe.....**

Kumb.Na.BSS/KTC/J.I F.I/2021

Mzazi wa

Shule ya Msingi

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA SHULE YA SEKONDARI BUGISHA HALMASHAURI YA
MJI KAHAMA MKOA WA SHINYANGA MWAKA 2021**

1.0: UTANGULIZI

Uongozi wa shule ya sekondari Bugisha unayofuraha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kуjiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka wa masomo Shule ipo umbali wa km 15 kutoka makao makuu ya HALMASHAURI YA MJI KAHAMA, kata ya Mondo barabara iendayo SHINYANGA

Muhula wa masomo utaanza **tarehe** Unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe na mwisho wa kuripoti ni tarehe ndani ya siku saba. Mwanafunzi asiyeripoti hatua kali dhidi ya mzazi/mlezi zitachukuliwa na nafasi yake atapewa mwanafunzi mwingine mwenye sifa.

: MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

: Sare ya shule

a) WAVULANA

- Suruali mbili (02) rangi ya damu ya mzee zisibane.
- Shati nyeupe mbili kitambaa cha tatron mikono mifupi, sweta na tai rangi damu ya mzee,t-shirt rangi ya kijivu yenye kola (form six).
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kamba visigino vifupi na Soksi ndefu nyeupe.
- Faili la plastic moja (folder file) ambapo viambatisho A na B vimewekwa
- **Bukta** jozi mbili au tracksuit rangi nyekundu na **Raba** jozi moja kwa ajili ya michezo.

b) WASICHANA

- **Sketi** mbili rangi ya damu ya mzee, Shati nyeupe mbili kitambaa cha tatron mikono mifupi.
 - Sweta na tai rangi damu ya mzee,t-shirt rangi ya kijivu yenye kola (form six).
 - Viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye mikanda (sio vya kamba au visivyo na mikanda) visigino vifupi na Soksi ndefu nyeupe.
 - Faili la plastic moja (folder file) ambapo viambatisho A na B vimewekwa
 - **Bukta** jozi mbili au tracksuit rangi nyekundu na **Raba** pea moja kwa ajili ya michezo.
- c) Rangi ya hijab ifanane na sare ya shule.**

: MAJUKUMU YA MZAZI/MLEZI

- a) Kumwandalia mwanafunzi sare ya shule na ya michezo.
- b) kumwandalia vifaa vya kujifunzia vikiwemo daftari,kalamu ,mathematical set n.k
- c) Kumpatia Chakula mwanafunzi wa kutwa kwa kuchangia chakula shulenii,
- d) Matibabu , kama hana bima ya afya,mzazi aje na Tsh 5,000/= ya bima ya afya iliyoboreshwa (bima ya afya ni lazima kwa mwanafunzi kuwa nayo).fedha itakusanya shulenii siku ya kufungua shule

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI BUGISHA

.....
**MPENA, M.W
MKUU WA SHULE**

Kiambatisho A

**SHULE YA SEKONDARI BUGISHA
(PERSONAL PARTICULARS) FOMU YA TAARIFA
BINAFSI**
(IJAZWE KWA HERUFI KUBWA)

NYONGEZA (B)

1. Jina kamili la mwanafunzi
2. Tarehe ya kuzaliwa(ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa).

3. Mahali unapoishi kijiji.....kitongoji.....
4. Utaifa.....kabila.....
5. (a) Anwani kamili ya nyumbani (Yaani ya mzazi).....
 (b) Jina la baba/mlezi.....Hai /amefariki (kata isiyohusika).
 Kazi yake.....Mahali anapoishi.....
 Anwani yake.....Namba ya simu.....

6. (a) Jina la mama/mlezi.....Hai /amefariki(kata isiyohusika).
 Kazi yake.....Mahali anapoishi.....
 Anwani yake.....Namba ya simu.....

7. Taja ndugu wasiopungua watano wa karibu wanaoweza kutoa msaada kwa mwanaao.

S/Na	JINA KAMILI	UHUSIANO	KAZI	MAHALI	Na. YA SIMU
1.
2.
3.
4.
5.

(b) Wewe ni mtoto wa ngapi kuzaliwa?

8. Mbali na masomo taja aina ya michezo unayopenda kucheza.

(i)..... (ii).....

9. AHADI YA MZAZI/ MLEZI

Mimi mzazi /mlezi wa.....Naahidi kumnumunilia mahitaji yote ya shule kwa muda unaotakiwa, kuhakikisha nampatia chakula shulenii pamoja na **BIMA** ya afya na awe anahudhuria shule kila siku.

Saini ya mzazi/mlezi.....tarehe.....

10. AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi..... Naahidi kuzifuata sheria na kanuni zote za shule ikiwa ni

pamoja na kuhudhuria siku zote za masomo bila kukosa na kuwa nikikosa bila taarifa niadhibiwe kwa mujibu wa kanuni, sharia na taratibu za shule

Saini ya mwanafunziTarehe.....

FOMU HII IGONGWE MUHURI WA AFISA MTENDAJI WA KATA**MUHURI UGONGWE HAPA**

Kiambatniso B

KAHAMA TOWN COUNCIL

BUGISHA SEC.SCHOOL,P.O.BOX 873, KAHAMA

MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by a Government Medical Office in respect of FORM 1/5 Entrants

Pupil's full name sex Male/Female

Blood count (Red and White)

Stool Examination

Analysis

Syphilis Test

Eye Test

Ears

Chest

Spleen

Abdomen

Pregnancy

ADDITIONAL INFORMATION:

e.g. Physical defects or impairments infections or inherited diseases.

.....
.....
.....

I Certify that the above student is fit/unfit for admission for further secondary education

Signature

Designation

Station

Date

Rubber Stamp

OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA MJI WA KAHAMA

SHULE YA SEKONDARI BUGISHA:

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Makosa ambayo Mwanafunzi akifanya anaweza kufukuzwa shule mara moja ni kama ifuatavyo

1. Wizi.

2. Uasherati.

3. Ulevi wa aina yoyote ile.

4. Uvutaji wa aina yoyote ile.

5. Makosa ya jinai.

6. Kupiga au kupigana.

7. kuharibu kwa makusudi mali ya shule.

8. Kudharau Bendera na alama nyingine za taifa.

9. Kuoa au kuolewa.

10. Kubeba ujauzito/mimba

11. Kusababisha mimba ndani au nje ya shule.

12. Kugomea adhabu kwa makusudi.

13. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.

Mwanafunzi anatakiwa;

1. Kuwahi shulen i kila siku.

2. kuongea kiingereza wakati wote awapo shulen.

3. Kamera, simu za mkononi na redio haviruhusiwi shulen, vikikamatwa mwanafunzi atachukuliwa hatua kali. Ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa.

4. Lugha za matusi haziruhusiwi shulen na atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kidhamu.

5. Wavulana kunyoa mitindo ya kihuni kama vile panki, kiduku au kunyoa upara na kufuga ndevu hawaruhusiwi kabisa..

6. **Usafi binafsi na kutunza mazingira ni jambo la lazima kwa kila mwanafunzi.**

7. Mwanafunzi hatakiwi kuvalaa mapambo aina yoyote kama vile, heleni, bangili, mkufu, banio la nywele n.k. Pia

hawaruhusiwi kufuga kucha au kupaka rangi.

8. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

9. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule.

10. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

11. Kufanya mitihani yote ya nje na ndani kama ilivyopangwa

